

## HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri)

Email:

[ded.mkalamadc@singida.go.tz](mailto:ded.mkalamadc@singida.go.tz)



Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,  
S.L.P 1007,  
**SINGIDA.**

Simu Na. 026-2964000

**Kwa kujibu, taja:**

Kumb.Na.MDC/CF.10/1/A/

17/03/2020

### **TANGAZO LA UWEKEZAJI KIWANDA CHA KUSINDIKA MAZAO YA BUSTANI ZABUNI LA LGA/147/2019/2020/NS/GUMANGA/01**

Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama ina kiwanda cha kusindika mazao ya Bustani katika Kijiji cha Gumanga, inatangaza nafasi ya kumpata Mwekezaji atakaye hudumu katika Kiwanda cha kusindika Mazao ya Bustani Gumanga. Hivyo mwekezaji mwenye sifa anakaribishwa kuomba kazi tajwa hapo juu.

**MAHALI KILIPO:** - Kiwanda kipo kijiji cha Gumanga, wilaya ya Mkalama, kilomita 16 kutoka Nduguti makao makuu ya Wilaya

#### **A UWEZO WA KIWANDA.**

Kiwanda kina uwezo wa kusindika tomato sauce/chill/paste (chupa 900mls) kiasi cha chupa 140,740 kwa mwaka

#### **B FURSA ZINGINE ZILIZOPO.**

- Kusindika Mvinyo wa nyanya (chupa 750mls) kiasi cha chupa 26,667 kwa mwaka
- Kusindika vitunguu kwa kukausha (pakti za 250gm) pakti 9,240 kwa mwaka
- Kukausha majani ya maboga (pakti za 250gm) pakti 13,860 kwa mwaka
- Kuna wakulima wengi wa nyanya na vitunguu ambao wapo tayari kulima mazao ya bustani.

- Barabara kuu za Mikoa (TANROADS) zinapitika muda wote katika mwaka.

### C. Raslimali zilizopo kiwandani

Na.	Aina ya kifaa	Idadi
1.	Mashine (Complete tomato processing machine)	1
2.	Mzani mkubwa (500kg)	1
3.	Mizani midogo (wa gramu)	2
4.	Kaushio la kutumia jua	1
5.	Kuna umeme na maji	
6.	Vitendea kazi kiwandani (ndoo, visu, tanki la maji n.k)	-
7.	Kuna eneo kubwa la kutosha kwa ajili ya kupanua kiwanda na kuhifadhia malighafi	
8.	Kuna jengo kubwa la kiwanda	1

#### 1. Kazi zitakazofanyika ni kama ifuatavyo:

- Kutengeneza tomato source, chill source, na tomato paste, tomato wine.
- Kufanya shughuli zote za uendeshaji wa kiwanda
- Kulipa kodi zote zinazotakiwa na Serikali
- Mwekezaji aonyeshe uwezo na uzoefu katika shughuli tajwa hapo juu
- Aoneshe kiasi cha ushuru atakachochangia kama marejesho katika Halmashauri.

#### 2. Sifa za Mwombaji

- Awe ana uzoefu na kazi zinazofanana na zilizotangazwa hapo juu.
- Mwekezaji anatakiwa kuonyesha kazi ambazo amewahi kuzifanya.
- Awe na mtaji wa kutosha kwa maana ya Raslimali watu na vitendea kazi muhimu (awe na uwezo wa kulipa wafanyakazi )
- Awe amesajiliwa na Mamlaka zinazohusika kama TRA, OSHA n.k

